HISTORIA FUPI YA KANISA KUU LA MTAKATIFU YOSEF



Mhashamu Jude Thaddaeus Ruwa'ich
Askofu Mkuu Jimbo Kuu la Dar es Salaam



Padre Dennis Wigira



HISTORIA YA PAROKIA

Kanisa la Mt. Yosef lilipandishwa hadhi ya kuwa Parokia 1889 likiwa ni Kanisa pekee kabisa kuwa Parokia katika Jimbo la Dar es salaam

Makazi ya mwanzo ya Wamisionari

Mwanga wa kufikiwa na Imani ya Kikatoliki kwa watu wa Dar es salaam ulipatikana pale walipofika Padre Bonifacius OSB na Mabruda wawili hapa Dar es salaam mwezi Novemba 1889. Hawa walifika kwa Bwana Wassermann Mkuu wa Wajerumani wa Dar es salaam wa wakati huo. Baada ya muda mfupi walipewa nyumba mbili zilizokuwa hazikaliwi kutokana na kuharibika sana. Nyumba hizi zilitengenezwa na mwezi April 1890 walizihamia, nyumba hizi zinaonekana hadi sasa, zipo kwenye kona ya City drive na Mtaa wa Misioni na kulia kwake walikaa Mapadre

UJENZI WA KANISA LILILOPO SASA

Ujenzi wa kanisa la Mt. Yosefu ulianza mwaka1896 wakati wamisionari walipopewa kiwanja na Serikali ya kikoloni ya Wajerumani, moja ya masharti ilikuwa wajenge jengo zuri na la maana. Hatua hii ndiyo iliyozaa baraka ya kuanza rasmi kwa ujenzi wa Kanisa tarehe 5, Desemba 1897. pale liliposimama Kanisa. Ramani ya kanisa ilichorwa na Arkitekti Schurr kutoka Munich Tar 2 Julai.1897. wajenzi walikuwa Bruda Selesius O.S.B na Bruda Elias O.S.B



Padre Maurus Hartmann OSB

Alizaliwa tar 21.11.1865 kama mtoto wa nne wa Wazazi wake. Baada tu ya kuzaliwa , siku chache baadaye mama yake alifariki. 1887 alipomaliza tu sekondari aliingia Utawa wa St Ottilien. Alipata Upadri 1890. Na 1891 alipewa cheo cha wakili wa Mkuu wa utawa(Upriori). 1894 Pd. Maurus alikabidhiwa cheo cha mkuu wa Mision na mkuu wa watawa. Pd. Maurus alikuwa hodari na aliyejituma.



Eneo la kiwanja lilipojengwa Kanisa 1888

JIWE LA MSINGI


Jiwe la msingi liliwekwa tarehe 13 Machi 1898 na Bwana Liebert, Gavana wa Afrika Mashariki ya Kijerumani (Deutsch Ostafrika)

Tar 2 Julai.1897 Bruda Ludger ambaye alikuwa anaishi Kurasini alihamia eneo la Kanisa Kuu kwaajili ya kuanza shughuli za ujenzi wa Kanisa Tarehe 5 Desemba. 1897

Juhudi kubwa za ujenzi wa Kanisa la Mt Yosefu zilifanywa na Padri Maurus Hartman. Miongoni mwa alama zilizoachwa na P, Maurus Hartmann kama sehemu ya juhudi zake zinazoonekana mpaka leo ni ujenzi wa Kanisa Kuu la sasa la Mt. Yosefu.

Kazi ya ujenzi ilienda kwa kasi na baada ya miezi mitano kati ya Mwezi ya Nane hivi 1898 kuta zilifikia dirishani. Mwaka mmoja baadae ujenzi wa kuta ulimalizika. Mikingio ya boriti na (kenchi) kwaajili ya paa ziliagizwa kutoka ulaya , Mnara ulijengwa pia. Juhudi kubwa za ujenzi wa Kanisa la Mt Yosefu zilifanywa na Padri Maurus Hartman. Padre Maurus Hartmann Mtume wa Injili, alikuwa akihudumu katika Parokia ya Mt. Yosef, alifika Dar es salaam tarehe 24 Juni.1894 akiongozana na Mabruda wanne na masista sita.

Baada ya miezi mitano kufikia Agost 1898 kuta zilifikia dirishani. Mikingio ya boriti na (kenchi) kwaajili ya paa ziliagizwa kutoka ulaya, Mnara ulijengwa pia. Mnamo tarehe 28 Machi 1901 Bruda Eliasi alipata ajali ya kuanguka toka juu kwenye mnara na kufa akiwa katika harakati za ujenzi, Mwezi Desemba 1901 ujenzi wote wa nje ulikuwa umekamilika na kubaki ule wa ndani.




Tarehe 21Februari, 1898, Bruda Ludger alifariki dunia, badala yake Bruda Selesius O.S.B alipokea kazi ya kusimamia majengo akisaidiana na Mabruda wenzake Gereon, Livinus na Elias. Mnamo Tarehe 28 Machi 1901 Bruda Eliasi alipata ajali ya kuanguka toka juu kwenye mnara na kufa akiwa katika harakati za ujenzi, lakini tukio la kifo halikusababisha kazi isimame bali iliendelea, na mwezi Desemba 1901 ujenzi wote wa nje ulikuwa umekamilika na kubaki ule wa ndani

Kubarikiwa kwa Kanisa la Mt. Yosef

Tarehe 4 Februari 1903 Kanisa lilibarikiwa na Padre Thomas Spreiter O.S.B, na shughuli za Maadhimisho zilifanyika zikitanguliwa na Misa takatifu ambayo iliongozwa na Padre Thomas Spreiter O.S.B.
Altare ya kwanza ililetwa ikiwa ni zawadi kutoka jumuiya ya Wagoa ambayo iliwekwa upande wa kulia wa Kanisa kwa heshima ya Mt. Sabastiani.
Altare kubwa ya mbele ilitoka Ujerumani ikiwa ni zawadi toka kwa Kaisari wa Ujerumani maarufu Caesar Wilhelm II. Jina lake kamili Wilhelm Victor Albrecht. Altare hii ikiwa ni ya marumaru ililetwa katika awamu mbili. Kuwasili kwa Altare ndio kulikamilisha ujenzi wa Kanisa la Mt. Yosef.

13 March, 1906 Baba Mt. alimteua Padre Thomas Spreiter kuwa Askofu wa Jimbo la Dar es salaam miezi michache baada ya kifo cha Askofu shahidi Kassian Spiess



Mhs. Thomas Spreiter, Askofu Jimbo la Dar es Salaam (1906 - 1920)

Mhs.Thoms Spreiter



Mhs. Kassian Spiess. Askofu wa kwanza Jimbo la Dar es Salaam(15.09.1902 - 21.08.1905)

UJENZI WA NDANI

Kuunganishwa kwa maboriti kulifuatiwa na kuwasili kwa kengele nne tarehe 16 julai 1907. Kengele hizi zilibarikiwa na na kutundikwa katika mnara kwa heshima ya Mt. Yosef, Mt. Maria, Mt. Ambrosius na Mt. Augustine.

KANISA LINAWEKWA WAKFU

Kuwekwa kwa Altare kulifuatiwa na tukio muhimu tarehe 15 Oktoba 1908. Askofu Thomas Spreiter O.S.B aliliweka kanisa wakfu, na hapo ndipo kanisa lilikuwa kamili au tayari kutumika. Altare ya Mt. Sebastian iliwekwa wakfu baadaye na mwaka 1972 Altare hii iliondolewa kabisa na mahali pale kilijengwa kisima cha ubatizo ambapo kipo mpaka leo.
Na mwaka 1911 sanamu ya Bikira Maria wa mateso iliwekwa. Taarifa zinaonyesha kuwa sanamu hii ilichongwa kwa kwa kutumia mti wa mvule kutoka kusini mwa Tanzania

Nyumba ya Mapadre

Nyumba ya mapadre iliyoko pia inasisimua historia yake. Katika mwaka 1896 Padre Maurus Hartman O.S.B alinunua kiwanja kutoka kwa muhindi mmoja, mahali hapo kulikuwa na Msikiti. Ujenzi ulifanyika na kukamilika mwaka 1905 na mapadre waliweza kuhamia. Kuhamia kwa

mapadre katika jengo hilo kutoa nafasi kwa masista kutumia nyumba walizohama kwaajili ya shule ya bweni

NYUMBA YA MASISTA

Mwaka 1908 Askofu alinunua nyumba na bustani karibu na kanisa. Hapo ilijengwa nyumba ya Masista iliyokamilika mwaka 1915 na kuhamiwa nao tarehe 1 Mei mwaka huo huo, hivyo waliyahama makao ya kona ya city Drive na mtaa wa Mission

Maparoko Parokia ya Mt. Yosefu 1921 – 1926

1921 Padre Gabriel Zelger
Padre Clemens Studer
1923 Padre Meinrad Schuler
1926 Padre Hieronymus Schildknecht

Matukio Muhimu

1924 Kigango cha Kariakoo kilianzishwa na Padre Meinrad OFM Cap.
1927 Parokia ilipata gari la kwanza aina ya Box Body kutoka Ulaya.
1928 Mei 29, Majengo ya Nyumba ya Masista ya Mt. Yosef yalibarikiwa
1930 Kanisa la Mt. Fransiscus la Kariakoo lilibarikiwa ambalo ndilo kanisa la kwanza nje ya Kanisa la Mt. Yosefu, Kanisa hilo lipo sehemu maarufu inayoitwa Mission Quarter
1953 Machi 25 Jimbo Kuu la Dar es salaam linazaliwa. Mhashamu Edgar Aristide Maranta O.F.M ndiye alikuwa Askofu Mkuu wa kwanza Jimbo Kuu la Dar es salaam



MHASHAMU EDGAR A. MARANTA MKAPUCHINI, ASKOFU MKUU, JIMBO KUU LA DAR ES SALAAM (27. 3. 1930 - 1968)

MADARAJA YA KICHUNGAJI

1923 Juni 24 Askofu Gabriel Zelger OFM aliwekwa Wakfu
1930 Agosti 17 Askofu Edgar Maranta OFM CAP aliwekwa Wakfu na ambaye alikuwa Askofu Mkuu wa Jimbo 1969
1949 Agosti 21. Ulifanyika Upadrisho wa Pd. Otto Frisch
1952 Machi 30. Mapadre Dennis na Birch waliadhimisha Misa ya kwanza baada ya kupata Upadrisho Kipalapala. Hawa walikuwa wamepokelewa kutoka madhehebu ya ki Anglikana.
1952 Agosti 15 Padre Hermenegild Muba alipata Upadrisho

1956 Machi 18. Padre Valerian Fataki alipewa Daraja la Upadre1969 Des 14 Ni siku ambayo Padre Callisti Nyambo alipewa Daraja ya Upadre.

Ukarabati wa Kanisa la Mt. Yosef

Mwaka 1932 Kanisa Kuu la Mt. Yosefu lilifanyiwa ukarabati tena upya na kufanya mwonekano wake kuvutia. Pia mwaka 1949 Paa la jengo liliezekwa upya kwa kubadilisha aina ya mbao aina ya Mvule.

Mabench yanayotumika katika Kanisa la Mt. Yosefu hivi sasa yalipatikana mwaka 1965. Lakini pia kutokana na mabadiliko ya kilitrujia, Altare iligeuzwa na kuwaangalia waumini.

Hali kadhalika, mwaka 1968, Kanisa lilipakwa tena rangi kwa nje na kulifanya kuwa na mwonekano mzuri kabisa kama wakati wa upya wake.

Kanisa Kuu la Mt. Yosefu

Kufikia 1953 Dar es Salaam ilikuwa na Parokia moja tu ambayo ni Mt. Yosefu. Kurasini, Msimbazi, Pugu na mbagala vilikuwa vigango tu, lakini katika mfululizo wa miaka kadhaa vigango vingine viliongezeka mpaka kufikia 12 na vingine vikiwa kama msingi wa Parokia. Mapadre wa Parokia ya Mt. Yosef ndio walio hudumu katika Vigango hivi.

Vigango

Ndani ya kipindi cha mwaka 1954 Parokia ya Mt. Yosefu iliweza kuzaa vigango vingine ambavyo miongoni mwao ni;

1. Kurasini 2.Msimbazi. 3. Pugu 4.Mbagala 5. Kariakoo na 6.Chang'ombe

MATUKIO MUHIMU


- 1925 Shirika la Moyo Mtakatifu wa Yesu lilianzishwa na Padre Hieronymus OFM cap. Wakati huo akiwa Paroko wa Mt. Yosefu

- 1930 Kanisa la Mtakatifu Fransiscus la kariakoo lilibarikiwa ambalo ndilo kanisa la kwanza nje ya kanisa la Mtakatifu Yosefu. Kanisa hilo liko sehemu inayoitwa maarufu kama mission Quarters.

- Tarehe 13 Agosti 1933.Palifanyika Mkutano wa kwanza wa chama cha Vincent wa Paul.
- Tarehe 24 Julai 1934. Kulitolewa ruhusa ya kuanzishwa utawa wa Mt Francisco wa Asisi.
- Mwak 1939 Mama Adel Quinn kutoka Dublin Ireland alitembelea Dar es salaam ili kuanzisha na Kuimarisha Vikundi vya Regio Maria

- Tarehe 4 Machi,1962 Kulifanyika Mkutano wa kwanza wa Halmashauri ya Walei mara baada ya kuunda katiba

- 1969 Mei. Mwadhama Laurian Rugambwa alitawazwa kuwa Askofu Mkuu wa Jimbo la Dar es Salaam. Alipokea Wadhifa huo kutoka kwa Askofu Mkuu Edgar Maranta OFM




Mwadhama L. Kard. Rugambwa Askofu Mkuu, Jimbo Kuu la Dar Es Salaam Tar 25 Mei, 1968 - 1992

- 1971 Aprili 7, Msgr. Dennis alifariki katika nyumba ya Mapadre
- 1971 Jan 23. Mkutano wa kwanza wa Legio Maria ulifanyika Keko Mwanga
- 1974 Ilianzishwa Ibada ya kuombea miito na Chama cha Moyo Mtakatifu wa Yesu
- 1980 Agost. 17 ilifanyika Ibada ya kuweka nadhiri ya maisha kwa Sista Clarina wa St. Joseph's Convent.
- 1983 Agosti 5. Sherehe ya Jubilei ya miaka 25 ya Upadre wa Padre Mansuetus Ilifanyika alipotimiza miaka 25 Tar 29 Julai 1983.

Maparoko waliohudumu Kanisa Kuu la Mtakatifu Yosefu 1969-1992

PD CALLIST NYIMBO	1972-1977	PAROKO
PD MANSUETUS	1972-1977	PAROKO MSAIDIZI
PD MANSUETUS	1977-1979	PAROKO`
PD FRANCIS NYONI	1977-1979	PAROKO
PD. MASEKO	1977-1979	PAROKO MSAIDIZI
PD. HENRY KABUKALE	1983-1987	PAROKO MSAIDIZI
PD. THOMAS TIBAINUGUKA	1986-1996	PAROKO MSAIDIZI



Padre Mansuetus

Wageni

- 1943 Askofu Spellman kutoka New York Marekani aliudhuria maadhimisho ya Sikukuu ya Ekaristi Takatifu. Alifurahia sana maandamano ya Ekaristi
- 1963 Mwl. Nyerere alihudhuria Ibada ya Misa ya Wafu ya Marehemu Papa Yohane wa XXIII

Madaraja ya Upadre

1972 Feb. Mwadhama Laurian Kardinali Rugambwa alitoa Daraja la Ushemasi kwa Maflateri Deogratias Mbiku, Juvenalis Muba na Ludovick denkeri

1981 Nov 22 Padre Camillius Luambano alipewa Daraja la Upadre

1987 Jun 13 Padre George Say Alipewa Daraja la Upadre

1987 Oktoba 4. Nadhiri ya kwanza ya Masista wa Dada Wadogo wa Mt. Fransisco wa Asizi ziliwekwa

1971 – 1976 Pd. Callistus Nyambo anachaguliwa kuwa Paroko wa Kanisa Kuu la Mt. Yosef



Grotto ya Mama Bikira Maria kwa muonekano wa mwanzo 1987 kabla ya kubomolewa na kujengwa upya. Ilijengwa Chini ya usimamizi wa Padre Mansuetus Blinkoff 1987

Jumuiya

Parokia in jumuiya zipatazo kumi na tisa (19) zikihusisha wenye asili ya Asia (Wagoa) jumuiya zipatazo Tisa (9) na jumuiya (10) za waamini wenye asili ya Kiafrika. Jumuiya hizi zinasali pamoja, na zote zinautaratibu wake


Zipo Jumuiya ndogo ndogo za wanaozungumza lugha ya Kisawhili na lugha ya Kiingereza na Kigoa, kimsingi Jumuiya hizi zilianzishwa Mwaka 2003 chini ya Paroko wa wakati huo Pd.Joseph Matumaini.

Kupitia jumuiya hizi, changamoto mbalimbali hutatuliwa urahisi mfano zile za ndoa, Ushiriki mdogo katika masuala ya kikanisa, Malezi ya familia, elimu haswa kwa vijana, Umasikini na Maingiliano ya Kiimani.

Sio wote ambao waliweza kuja kusali Parokia ya Mt. Yosefu, baadhi yao walipendelea kusali



Grotto ya Bikira Maria iliyopo sasa



Kapela ya Mt. Yosef

Vyama vya Kitume

Kuna ushirikiano mkubwa kati ya uongozi Hierakia na waamini walei kupitia Kamati Tendaji za walei Parokia na Jumuiya ili kusaidia kufanikisha majukumu mbalimbali ya kazi za Kichungaji za siku hadi siku kwa kushirikiana na Vyama Mashirika na Jumuiya za kitume (VMJ) kama vile; **Utoto Mtakatifu** chini ya Shirika la Kipapa la Utoto Mtakatifu (PMS), **VIWAWA** hawa ni Vijana Wakatoliki Wafanyakazi. Wengine ni **UWAKA, WAWATA, Moyo Mtakatifu wa Yesu, UKWAKATA, Minitrant** (Wahudumu wa Altare), **Utume wa Fatima, Rozali Hai na** Jumuiya ya Wazazi na walezi wa Maflateri **(JUWAMA)** ambayo chimbuko lake ni Parokia ya Mtakatifu Yosefu.


Kanisa Kama Kituo cha Hija

Kanisa Kuu la Mt. Yosefu ni Kanisa la hija. Ni sehemu ambayo ina maandalio kwaajili ya sala kwa Mama Bikira Maria, Mtakatifu Yosefu na sala kwa Yesu wa Ekaristi. Ziko pia misa kila siku za juma, -Jumatatu mpaka Ijumaa na kwa utaratibu uliopangwa kwa siku za jumamosi na Jumapili na kwa matukio muhimu.

Pia zipo Sakrament mbalimbali zinazotolewa kwa kadiri ya utaratibu uliowekwa. **(Ubatizo, Komunio, Kipaimara, Ndoa, Upakao wa wagonjwa na Sakramenti ya upatanisho- Kitubio)**



MARGARET T. IKONGO
MWENYEKITI



PATRICK MBEDULE
MAKAM M/KITI



LIMA D'SILVA
KATIBU



Kamati Tendaji Halmashauri Walei
Parokia ya Mt. Yosefu 2026



IVAN C. KIHAMA
KATIBU MSAIDIZI



SIMON BYANYUMA
MTUNZA FEDHA